# Nyenzo za Huduma baada ya Kubakwa

KILA SAA INAYO 72 PITA NI MUHIMU
Kasi ni Lazima.

Together for girls
Ending violence against children

Kuna nyenzo nyingi zilizopo za kutoa mwongozo, mafunzo, na taratibu bora za kufuata katika kuanzisha huduma na itifaki za baada ya kubakwa. Nyenzo hizi zinaweza kuwasaidia viongozi wa ngazi ya kitaifa, kisekta, na kijami kuchukua hatua kuhusu huduma za baada ya kubakwa, na kuhakikisha kwamba kuendelea kuongezeka kwa huduma hizo kunaendana sambamba na uhamasishaji wake.

*>> Bonyeza mistar ya rangi ya machungwa **kupata nyenzo za kwenye mtandano.***

## MWONGOZO

**Mwongozo wa Shirika la Afya Duniani kuhusu Usimamizi wa Matibabu:** Rasmi vya utoaji wa huduma baada ya kubakwa katika vituo vya matibabu.(Kurasa hazipatikani kwa kiswahili.)

**Maelezo Muhimu kwa Wanawake na Wasichana Waliotendewa Ukatili-Vigezo muhimu na Mwongozo wa Ubora (UNWomen, UNFPA, WHO, UNDP, UNODC):** Taarifa hii inaorodhesha huduma muhimu zinazohitaji kutolewa na wahudumu wa afya, huduma za kijamii, Polisi na idara za sheria na pia mwongozo wa kuratibu utoaji wa huduma muhimu, na usimamizi wa mchakato na mbinu za uratibu. (Kurasa hazipatikani kwa kiswahili.)

**Huduma kwa Waathirika wa Unyanyasaji wa Kingono:** Hii ni nyenzo inayoweza kuenezwa kwa njia nyingi za kisasa, na inajumuisha mafunzo kwa wahudumu wote wa ki-afya, na ukaguzi wa kusaidia kutathmini uwezo wa sasa hivi wa kila kliniki katika kutoa huduma. Pia kuna mwongozo wa kufuatilia na kutathmini huduma punde zinapoanzishwa. Zipo katika lugha za Kiingereza, Kifaransa na Kiarabu. (Kurasa hazipatikani kwa kiswahili.)

**Usimamizi wa Matibabu ya Watoto na Vijana Walionyanyaswa Kingono:** Vigezo vya Kuzingatia katika kutumia Mpango wa PEPFAR : Taarifa hii inatoa mwongozo kuhusu huduma kwa watoto baada ya kubakwa. Ingawa mwongozo huu uliandaliwa kutumika katika mpango maalum wa Rais wa Marekani wa kupambana na Ukimwi (PEPFAR), serikali za mataifa zinaweza kujumuisha yaliyomo katika mwongozo wao wa kitaifa. (Kurasa zinapatikana kwa Kiswahili.)

**Uimarishaji wa Uhusiano Baina ya Huduma za Kimatibabu na Huduma za Kijamii kwa Watoto na Vijana Walionyanyaswa Kingono:** Huu ni Mwongozo wa Kutoa Huduma kwa Watoto na Vijana Walionyanyaswa Kingono, ambao umetayarishwa kuwasaidia wahudumu wa kiafya na wasimamizi kuelewa na kuwezesha ushirikiano na huduma za kijamii, na kuhakikisha watoto wanaotendewa ukatili wanapata msaada zaidi ya matibabu, na kubadilika kwa tamaduni za kijamii zinazojenga ukatili. (Kurasa hazipatikani kwa kiswahili.)

**Mwongozo kuhusu Tiba ya Kuzuia Maambukizi ya Virusi vya Ukimwi Baada ya Kubakwa, na Matumizi ya dawa aina ya Co-trimoxazole Prophylaxis zinazotibu maambukizi mengine yenye uhusiano na virusi vya HIV kwa watu wazima, vijana na watoto:** Taarifa hii (iliyochapishwa Disemba 2014) ni nyongeza ya mwongozo uliotolewa 2013 kuhusu matumizi dawa za kufubaza virusi vya HIV katika kutibu na kuzuia maambukizi ya HIV. Baadhi ya mapendekezo yaliyomo ni tiba ya dharura ya kuzuia maambukizi ya HIV (post-exposure prophylaxis) na pia dawa za kutibu maambukizi mengine yaliyo na uhusiano na HIV (co-trimoxazole prophylaxis) miongoni mwa watu wazima, vijana na watoto. (Kurasa hazipatikani kwa kiswahili.)

**Njia za Kushughulikia Ukatili unaotokana na Mshirika wa Ndoa au Mpenzi, na Unyanyasaji wa Kingono Dhidi ya Wanawake:** Mwongozo huu kutoka Shirika la Afya Duniani utawapa wahudumu wa ki-afya maelekezo yanayozingatia ushahidi kuhusu namna ya kushughulikia unyanyasaji unaotokana na mshirika wa ndoa au mpenzi, na unyanyasaji wa kingono dhidi ya wanawake. Pia unatoa ushauri kwa watunga sera, uratibu ulio bora na ufadhili wa huduma, na pia kuzingatia zaidi hatua za kuchukuliwa kuhusiana na unyanyasaji wa wa kingono na ukatili unaotokana na mshirika wa ndoa/mpenzi katika programu za kutoa mafunzo kwa wahudumu waki-afya. (Kurasa hazipatikani kwa kiswahili.)

**Huduma ya Afya kwa Wanawake Waliotendewa Ukatili na Mume/Mpenzi au Unyanyasaji wa Kingono: Mwongozo wa Matibabu:** Kitabu hiki cha mwongozo kutoka Shirika la Afya Duniani kinatoa maelekezo rahisi ya hatua na mapendekezo ya kusaidia wauguzi kutoa usaidizi wa ubora wa hali ya juu na huduma iliyokamilika kwa mwanamke aliyekabiliwa na unyanyasaji. (Kurasa hazipatikani kwa kiswahili.)

*Uendelee ukurasa zifuatazo >*

## MWONGOZO NA USHAHIDI UNAOHUSU NCHI

**Tathmini ya Hatua za Pamoja Zinazochukuliwa na Idara Mbali Mbali (Kituo Kimoja) Kuhusu Unyanyasaji wa Kijinsia katika Nchi za Kenya na Zambia:** Ushahidi wa muundo wa kituo cha pamoja kutoka Zambia na Kenya, iliyochapishwa 2012 na Shirika la kimataifa la Population Council. (Kurasa hazipatikani kwa kiswahili.)

**Huduma ya Baada ya Kubakwa katika Maeneo yasiyo na Nyenzo za Kutosha:** Mafunzo kutoka Mfano wa Kenya (Liverpool VCT): Taarifa ya sera kuhusu uanzishaji wa huduma iliyokamilika ya baada ya kubakwa. (Kurasa hazipatikani kwa kiswahili.)

**Mwongozo wa Kitaifa Kuhusu Usimamizi wa Unyanyasanji wa Kingono nchini Kenya:** Mfano wa mwongozo wa Kitaifa katika Usimamizi wa Matibabu. (Kurasa hazipatikani kwa kiswahili.)

## NYENZO ZA ZIADA

**Huduma ya Simu ya Dharura ya Kimataifa ya Msaada kwa Watoto (Child Helpline International):** Mataifa 142 yana huduma ya simu ya dharura ya kupiga kupata taarifa na maelekezo ya kuhudumiwa kimatibabu na huduma zingine. Pia kuna nyenzo za kusaidia katika kuanzisha na kusimamia huduma ya simu ya dharura kwa ajili ya kuwasaidia watoto. (Kurasa zinapatikana kwa Kiswahili.)

**Mtaala wa Matibabu kwa Watoto Walionyanyaswa (BRANCH Partners):** Mtaala huu, umetayarishwa kutumika na wahudumu waliopata mafunzo ya viwango vya juu sana na ujuzi wa kutibu, mawasiliano na kubaini magonjwa katika kuwahudumia watoto walionyanyaswa. Pamoja na mtaala kuna kitabu cha maelekezo kwa wanaofunza na wanaoshiriki mafunzo, ukaguzi, na uhakiki wa mafunzo. BRANCH Partners pia wanatoa nyenzo za kutoa mafunzo kwa kituo cha pamoja cha kutoa huduma. (Kurasa hazipatikani kwa kiswahili.)

**Unyanyasaji wa Kijinsia na HIV: Mwongozo wa Kujumuisha Kuzuia Unyanyasaji wa Kijinsia na Kuitikia Katika Programu za PEPFAR:** Licha ya kuwepo ushahidi mkubwa kuonyesha kwamba unyanyasaji wa kijinsia ni chanzo na pia matokeo ya maambukizi ya HIV, programu na huduma zinazolenga kushughulikia matatizo hayo zinakosa uwiano. Mwongozo huu unatoa hatua ya kwanza ya wasimamizi na wahudumu wengineo katika kujumuisha mwitikio wa kimsingi kuhusu unyanyasaji wa kijinsia katika programu zilizopo za kupambana na HIV. (Kurasa zinapatikana kwa Kiswahili.)

**Mwongozo Kuhusu Nyenzo za Kupambana na Ukatili Dhidi ya Wanawake na Wasichana: (Benki ya Dunia, Taasisi ya Wanawake katika Chuo Kikuu cha George Wshington, Benki ya Maendeleo ya Inter-American, na Kituo cha Kimataifa cha Utafiti Kuhusu Wanawake:** Mwongozo huu unatoa taarifa za kimsingi kuhusu tabia na matokeo ya unyanyasaji dhidi ya wanawake na wasichana; mwongozo kuhusu namna ya kujumuisha unyanyasaji dhidi ya wanawake na wasichana katika sera na sheria, na pia programu na miradi inayoendeshwa na sekta mbali mbali. (Kurasa hazipatikani kwa kiswahili.)

**Kukomesha Ndoa za Utotoni, na Kutimiza Mahitaji ya Watoto Walioolewa: Dira ya Utekelezaji ya USAID:** Taarifa hii ya mkakati inaeleza kwa mukhtasari msimamo na mpango wa shirika la USAID wa kukomesha ndoa za utotoni na kutimiza mahitaji ya watoto walioolewa. Ina maelezo kuhusu mikakati iliyohakikiwa na hatua ambazo mafanikio yake katika kuzuia ndoa za utotoni yanaambatana na ushahidi, pamoja na taarifa kuhusu mambo mbali mbali yanayochangia ndoa za utotoni. (Kurasa hazipatikani kwa kiswahili.)

**Ukeketaji: Maelezo Kuhusu Takwimu na Upelelezi wa Uwezo wa Kuleta Mabadiliko:** Ripoti hii ya shirika la UNICEF ina maelezo ya jumla kuhusu idadi ya wasichana waliokeketwa katika mataifa 29 ambako utamaduni huo umejikita. Azma ya ripoti hii ni kuleta uelewa wa kina kuhusu ukeketaji, unaoweza kutumika katika sera na programu, kwa lengo la kutokomeza utamaduni huo. (Kurasa hazipatikani kwa kiswahili.)

**Mtandao wa Utekelezaji wa Sheria na HIV (LEAHN):** Hii ni njia ya kuwaunganisha watu wanaoshiriki katika kuzuia HIV, hususan wale wanaofanya kazi katika Nyanja za utekelezaji wa sharia na afya ya umma. Lengo la LEAHN ni kusaidia kujenga ushirikiano endelevu katika ngazi ya kimataifa na ngazi ya mashinani kufanya kazi kwa ufanisi mkubwa zaidi na makundi ya watu walio katika mazingira hatarishi, kwa mfano watu wanaojichoma kwa mihadarati, makahaba, wafungwa, wahamiaji, na wanaume wanaofanya mapenzi na wanaume wenzao. (Kurasa hazipatikani kwa kiswahili.)

TOGETHER FOR GIRLS GLOBAL PARTNERS:

EVERY HOUR MATTERS PARTNERS:

FOR MORE INFORMATION VISIT: **WWW.EVERYHOURMATTERS.ORG / WWW.TOGETHERFORGIRLS.ORG**